

## 21- Aayaat Katika Surwatul-Hajj Kuhusu Hajj

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

*A'uwdhu BiLLaahi Mina-shaytwaanir-Rajiym*

﴿ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ الَّذِي جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ سَوَاءً الْعِكِفُ فِيهِ وَالْبَادِ وَمَن يُرِدْ فِيهِ بِالْحَادِ بِظُلْمٍ نُّذِقْهُ مِن عَذَابِ أَلِيمٍ ﴾

25. Hakika wale waliokufuru na wanazuia (watu) njia ya Allaah na (pia wanazuia watu wasifike) *Al-Masjid Al-Haraam* ambao Tumeujaalia kwa watu kuwa ni sawasawa; kwa wakaao humo na wageni. Na yeyote anayekusudia humo kufanya upotofu kwa dhulma Tutamuonjesha adhabu iumizayo.

﴿ وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِي شَيْئًا وَطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴾

26. Na (taja) Tulipomwonyesha Ibraahiym mahali pa Nyumba (*Al-Ka'bah*, Tukamwambia): kwamba: “Usinishirikishe na chochote; na twaharisha Nyumba Yangu kwa wafanyao *Twawaaf*, na wanaosimama (kuswali) na wanaorukuu (na) kusujudu.

﴿ وَأُذِّنُ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴾

27. Na tangaza kwa watu Hajj; watakufikia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda, watakuja kutoka katika kila njia pana za milima zilioko mbali kabisa.

﴿ لَيْسَ لَهُدًى مِّنْفَعٍ لَهُمْ وَبَدَّكَرُوا أَسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَاتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْبَائِسَ الْفَقِيرَ ﴾

28. Ili washuhudie manufaa yao; na walitaje Jina la Allaah katika siku maalumu kwa yale Aliyowaruzuku kati ya wanyama wenye miguu minne wa mifugo. Basi kuleni humo, na lisheni mwenye shida fakiri.

﴿ ثُمَّ لِيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلِيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلِيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٣٨﴾ ﴾

29. Kisha wamalize taka zao (mwilini), na watimize nadhiri zao, na watufu kwenye Baytil-'Atiyq.

﴿ ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمِ حُرْمَتِ اللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَهُرْ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ وَأُحِلَّتْ لَكُمْ الْآتَعَمُ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ ۗ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣٩﴾ ﴾

30. Hayo, (yameamrisha) na yeyote anayeadhimisha vitukufu vya Allaah basi hivyo ni kheri kwake mbele ya Rabb wake. Na mmehalalishiwa (kula) wanyama wa mifugo isipokuwa wale mnaosomewa. Basi jiepusheni na *rijsi* (uchafu wa kuabudu) masanamu, na jiepusheni na kauli za uongo.

﴿ حُنَفَاءَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ ۗ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَكَأَنَّمَا حَرَّمَ مِنَ السَّمَاءِ فَتَخَطَّفَهُ الطَّيْرُ أَوْ تَهْوَىٰ بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٤٠﴾ ﴾

31. Muelemee haki kwa (kumwabudu Pekee) Allaah bila ya kumshirikisha. Na yeyote anayemshirikisha Allaah basi kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, wakamnyakua ndege au upepo ukamtupa mahali mbali mno.

﴿ ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمِ شَعْبِيرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٤١﴾ ﴾

32. Hivyo (ndivyo) na yeyote anayeadhimisha alama (za Dini) ya Allaah, basi hayo ni katika taqwa ya nyoyo.

﴿ لَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحْلَاهَا إِلَىٰ الْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٤٢﴾ ﴾

33. Katika hao (wanyama) mnapata humo manufaa mpaka muda maalumu. Kisha mahali pake (pa kuchinjwa) ni (karibu na) Baytil-'Atiyq.

﴿ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا لِيذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِّنْ بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۗ فَإِلَهُكُمْ إِلَهُهُ وَاحِدٌ ۗ فَلَهُ أَسْلِمُوا ۗ وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ ﴿٣٤﴾ ﴾

34. Na kwa kila Ummah Tumeweka taratibu za 'ibaadah ili watajse Jina la Allaah kwa yale Aliyowaruzuku ya wanyama wa miguu minne wa mifugo. Kwa hiyo *Ilaah* (Muabudiwa wa haki) wenu ni *Ilaah Mmoja* (Pekee); basi kwake Pekee jisalimisheni. Na wabashirie wanyenyekavu.

﴿ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَالصَّابِرِينَ عَلَىٰ مَا أَصَابَهُمُ وَالْمُقِيمِي الصَّلَاةِ وَبِمَا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٥﴾ ﴾

35. Ambao Anapotajwa Allaah nyoyo zao hushtuka (kwa khofu), na wanaosubiri juu ya yale yaliyowasibu, na wanaosimamisha Swalaah na katika vile Tulivyowaruzuku wanatoa.

﴿ وَالْبُدْنَ جَعَلْنَاهَا لَكُمْ مِّنْ شَعْتِيرِ اللَّهِ لَكُمْ فِيهَا خَيْرٌ ۗ فَأَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا صَوَافٍ ۗ فَإِذَا وَجَبَتْ جُنُوبُهَا فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ ۗ كَذَٰلِكَ سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾ ﴾

36. Na ngamia na ng'ombe Tumekufanyieni kuwa ni miongoni mwa alama (za Dini) ya Allaah; kwa hao mnapata kheri (nyingi). Basi tajeni Jina la Allaah juu yao wanapopangwa safu (kuchinjwa). Na waangukapo ubavu, basi kuleni kutoka humo, na lisheni waliokinai (hawaombi) na wanaolazimika kuomba. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (wanyama hao) kwa ajili yenu ili mpate kushukuru.

﴿ لَنْ يَنَالَ اللَّهُ خُومُهَا وَلَا دِمَاؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ ۗ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْنَاكُمْ ۗ وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾ ﴾

37. Haimfikii Allaah nyama zake wala damu yake, lakini inamfikia taqwa kutoka kwenu. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (hao wanyama) kwenu ili mpate kumtukuza Allaah (kusema: *Allaahu Akbar*) kwa yale Aliyokuongozeni; na wabashirie wafanyao ihsaan.